TANGAZO LA SERIKALI NA. 73 tarehe17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA BUGILANGOFI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Bugilangosi ya Mwaka 2023

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang’wale.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 460985.059MS, 9646619.663KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kaskazini katika uelekeo wa $109.36^0$ kwa umbali wa kilomita 0.86 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 461024.581MS, 9647480.409KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa $104.33^0$ kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 461742.825MS, 9647632.155KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa $153.6^0$ kwa umbali wa kilomita 0.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 461998.761MS, 9647565.811KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika

uelekeo wa $101.11^0$ kwa umbali wa kilomita 0.16 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 461990.811MS, 9647405.902KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika wa $86.11^0$ kwa umbali wa kilomita 0.48 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 461514.257MS, 9647457.004KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $89.14^0$ katika umbali wa kilomita 0.79 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 461447.999MS, 9646665.934KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa $119.46^0$ kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 461364.001MS, 9646613.491KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa $143.06^0$ kwa umbali wa kilomita 0.06 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba I yenye majira - nukta 461384.594MS, 9646560.597KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa $132.2^0$ kwa umbali wa kilomita 0.15 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba J yenye majira - nukta 461240.798MS, 9646509.604KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa $132.2^0$ kwa umbali wa kilomita 0.27 hadi ulipoanzia.''

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*